

Kuharibu Afya na Biashara Katika Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara

Na Busani Bafana



Bulawayo, Zimbabwe, Nov 20 2015 (IPS) - Mfanyakazi wa maabara, Herbert Mtopa anakusanya sampuli za kliniki katika Wilaya ya Shamva nchini Zimbabwe chini ya mradi wa CultiAF kuangalia jinsi wanawake na watoto wanavyoathirika na sumu ya *aflatoxins*.

Sumu ya *Aflatoxin* inazidi kuwa tishio kwa biashara, chakula na usalama wa afya katika Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara, ambapo wakulima wadogo wadogo wana changamoto ya kuzalisha chakula na kukabiliwa na mabadiliko ya tabia nchi, walisema watafiti.

Aflatoxins ni sumu inayosababisha kansa inayozalishwa na fangasi ambao wanapatikana katika ardhi. Sumu hiyo inakuwa tishio kwa chakula katika Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara ikiwa ni pamoja na mahindi, mihogo, mtama, viazi vikuu, mpunga, karanga na korosho.

Taasisi ya Kimataifa ya Kilimo katika Mazingira ya Kitropiki (IITA), yenye makao yake makuu nchini Nigeria imeongoza utafiti wa kupunguza sumu za aina hiyo barani Afrika kwa kuwa na mipango ya kiubunifu.

Kwa mujibu wa watafiti wa IITA, kutokana na watu kula sumu aina hiyo kumekuwa changamoto kubwa za afya na usalama wa watu wengi barani Afrika ambako kiasi kikubwa cha sumu aina ya *aflatoxin* kimethibitishwa kuwepo. Wakulima wengi wadogo wanashindwa kuzuia kuathiriwa na sumu hiyo wakati wa uzalishaji na uhifadhi wa mazao yao kwa kuwa wanashindwa kuwa na njia za gharam nafuu za kutambua sumu.

Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara kunapoteza zaidi ya dola milioni 450 kwa mwaka ambazo zingetokana na mapato ya biashara ya chakula kikuu kama vile mahindi na karanga kutokana na kuwa na sumu ya *aflatoxins*, watafiti waliambia IPS. Gharama za kiafya zinazotokana na watu kula sumu hiyo bila kujua zinafikia mamilioni ya dola katika ukanda ambao miundombinu ya afya imezidiwa uwezo.

Afrika ipo katika hatari ya sumu ambayo imehusishwa kupunguza kinga za mwili, kusababisha kansa ya ini na kudumaa kwa watoto. UNICEF inasema asilimia 40 ya watoto katika Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara wamedumaa au wana uzito mwepesi ikilinganishwa na umri wao jambo ambalo linaweza kusababisha kuwa na maendeleo duni ya ubongo wao.

Watafiti wanasema joto kali na hali ya ukame inasababisha kuongezeka kwa fangasi hao, wakati mbinu duni za kilimo na uhaba wa chakula kwa watu wengi katika Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara kunaongeza wao kuzidi kuathirika na sumu. Kwa kuongeza unyevunyevu mwingi ardhini wakati wa kuvuna ikiwa ni pamoja na misimu isiyokuwa na mvua kutokana na mabadiliko ya tabia nchi kunatengeneza mazingira ya kuongezeka kwa sumu.

“Mabadiliko ya tabia nchi yanatabiriwa kwenda na kuongezeka sumu aina ya *aflatoxin* katika chakula na mazao,” alisema Joao, akiongeza kuwa, “Kupungua kwa unyevunyevu kokote kule au kuongezeka kwa joto kunatarajiwa kuongeza tatizo la sumu ya *aflatoxin*.”

Mwaka 2009, IITA, Mfuko wa Teknolojia ya Kilimo Afrika (AATF), Taasisi ya Utafiti wa Kilimo ya Idara ya Kilimo ya Marekani (USDA-ARS) na wadau wengine walitengeneza teknolojia ya kibaolojia ya kudhibiti sumu, iliyopewa jina la AflaSafe kupunguza kuenea kwa sumu aina ya *aflatoxin* katika mahindi na karanga.

Udhibiti wa aflatoxin kibaolojia katika Afrika ulianza nchini Nigeria ambako Aflasafe kwa sasa ni bidhaa ambayo imesajiliwa. Kuna bidhaa ambazo zimetengenezwa kwa ajili ya nchi maalum kama vile Kenya, Burkina Faso, Senegal, Gambia na Zambia.

Katika mataifa yote sita ambapo udhibiti wa kibaolojia umefanyiwa majaribio tangu mwaka 2008 hadi leo hii, IITA ilisema wakulima wamefanikiwa hadi asilimia 99 kupunguza madhara ya sumu ya aflatoxin kwa kutumia Aflasafe katika mahindi na karanga.

“Faida zinazotokana na kutumia Aflasafe ni kubwa ikilinganishwa na gharama yake,” alisema Juliet Akello, mtaalam wa mimea na mwanachama wa timu ya IITA nchini Zambia. “Watu wanakula sumu ya *aflatoxin* kupitia vyakula kutokana na kukosa ufahamu, umaskini na serikali kutokusimamia vizuri ubora.”

Kimataifa sumu ya *aflatoxin* inafahamika kuwa tishio ambalo limepunguzwa kutokana na uwekezaji katika udhibiti wa usalama wa chakula. Wakulima wadogo barani Afrika wanategemea njia za jadi za hifadhi ya chakula na kutumia kemikali kuulia wadudu. Hata hivyo, njia hizi mara nyingi hazizuii kabisa wadudu na hivyo kujikuta wakipoteza mazao mengi wakari ambapo wanayahitaji zaidi.

Mbinu nyingi zinajaribiwa barani Afrika kudhibiti upotevu wa mazao kabla na baada ya kuvuna ikiwa ni pamoja na kuzuia mazao kuingiliwa na sumu ya *aflatoxin* kwa kutumia Aflasafe.

Nchini Zimbabwe, watafiti katika Chuo Kikuu cha Zimbabwe na shirika la *Action Contre la Faim* wanafanya kazi kwa pamoja na wanajamii katika wilaya mbili kuchunguza kama kuboresha hifadhi ya mazao kunaweza kupunguza sumu ya aflatoxin katika mahindi. Utafiti wa miaka miwili, unaofadhiliwa na mpango wa Kujenga Afrika ya Baadaye (CultiAF), mpango unaofadhiliwa na Kituo cha Utafiti wa Maendeleo ya Kimataifa cha Canada (IRDC) na Kituo cha Utafiti wa Kilimo Kimataifa cha Australia, pia watafanyia tathmii viwango vya sumu vinavyoathiri wanawake na watoto wachanga. Mradi huo umeanzisha maghala ya chuma na plastiki ili kuruhusu mahindi kuhifadhiwa katika mazingira yasiyoruhusu hewa kuingia.

Wakulima katika Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara wanakabiliwa na changamoto ya kukosa vifaa vya kukaushia mazao, huku wakulima wengi wa mahindi na karanga wakiacha mazao yao mashambani ili yakauke kabla ya kuvuna. Mara nyingine wanayahifadhi kabla hayajakauka vizuri, na hivyo kuyafanya kupata sumu ya aflatoxin kwa urahisi.

Uuzaji nje wa bidhaa za kilimo kama vile karanga kutoka Afrika kumeshuka kwa asilimia 20 katika kipindi cha miaka 20 iliyopita. Bidhaa hizo zimekuwa zikikataliwa baada ya kushindwa kufikia viwango vya soko la Ulaya la viwango vya sumu aina ya *aflatoxin* katika chakula kwa ajili ya kuliwa na binadamu, suala ambalo ni kikwazo kikubwa kwa biashara ya kimataifa.

Kwa mujibu wa Shirika la Kilimo na Chakula la Umoja wa Mataifa, ni nchi 15 tu za Afrika zimekuwa na udhibiti wa kiwango cha sumu ya *aflatoxin* ilipofika mwaka 2013.

Nchini Zambia, kwa mfano, karibu asilimia 100 ya siagi ya karanga katika masoko makubwa na madogo kati ya mwaka 2012 na 2014 iligundulika kuwa na viwango visivyokuwa salama vya sumu ya *aflatoxin*. Chini ya asilimia 30 ya unga wa karanga kutoka maduka makubwa na majumbani zilikuwa na viwango vya chini vya sumu vinavyokubaliwa na Umoja wa Ulaya.

Wakati ambapo nchini Kenya, nchi inayoongoza kwa sumu ya *aflatoxin* katika Afrika Mashariki, karibu watu 200 walifariki dunia baada ya kula mahindi yenye sumu ya *aflatoxin* kati ya mwaka 2004 na 2006. Karibu magunia ya mahindi milioni 2 yalikutwa kuwa hayafai kwa walaji kutokana na kuwa na kiasi kikubwa cha sumu ya *aflatoxin* mwaka 2010.

Meneja miradi wa IITA anayeshughulika na Aflasafe nchini Malawi, Dk. Joseph Atehnkeng, alisema kati ya asilimia 40 na 100 ya bidhaa za karanga nchini Malawi, zilikutwa na kiwango cha sumu kisichofaa kwa matumizi.

Mataifa yaliyokuwa yakiuza karanga kwa wingi nje ya nchi ya Msumbiji, Senegal, Gambia, Zambia na Malawi yamepoteza masoko ya EU, Marekani na Afrika Kusini kutokana na viwango vya sumu ya *aflatoxin* katika bidhaa zao, anasema mwanasayansi ya mimea wa IITA, Dk. Joao Augusto.

Tangu mwishoni mwa miaka ya 70, Msumbiji ilirikodi kiwango kikubwa cha kansa ya ini katika eneo la kusini mwa nchi ambako kumehusishwa na ulaji wa chakula chenye sumu ya *aflatoxin*, hasa karanga.

Kwa mujibu wa Mradi wa kikanda wa Udhibiti wa sumu ya Aflatoxin (PACA), ulioanzishwa mwaka 2009 kupunguza na kutokomeza sumu hiyo kwa kutumia mikakati ya

kiubunifu, kuna haja ya kuwa na sheria bora za kudhibiti sumu na nchi kuwa na viwango maalum.

Mtafiti Chapwa Kasoma kutoka Zambia, anaonya kuwa kama sumu ya *aflatoxin* haitadhibitiwa inaweza kupunguza kasi ya maendeleo katika Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara.

“Kama tunataka kukabiliana na umaskini katika sura zake zote; tunapaswa kukabiliana siyo tu na uhaba wa chakula lakini pia kuangalia ubora wa lishe,” Chapwa, ambaye pia ni msimamiaji wa kazi za mashambani katika shirika la Pioneer DuPont, aliiambia IPS. “Ni wazi kuwa sumu aina ya *aflatoxin* ni moja ya matatizo ya lishe bora.”

(End)